Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Forest Justice in Tanzania
FJT

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA
MJUMITA

# MRADI WA HAKI KATIKA MISITU AWAMU YA PILI

## MUHTASARI WA MRADI

**"Kila kijiji chenye msitu wa asili katika ardhi yake kina haki ya kuanzisha, kumiliki na kusimamia Msitu wa Hifadhi wa Kijiji kwa manufaa ya sasa na ya kizazi kijacho"**




### Utangulizi kuhusu mradi

Shirika la kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), wanatekeleza mradi wa Haki katika Misitu awamu ya pili kwa kipindi cha miaka miwili (2020 - 2021). Mradi unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Serikali ya Uingereza (DfID) kupitia programu ya uwajibikaji Tanzania kwa awamu ya pili (AcT 2), inayosimamiwa na KPMG. Wazo la mradi huu limetokana na msukumo kutoka kwa wadau wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) wakiwemo serikali za vijiji na Asasi za kijamii zinazotekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (USMJ) kwa lengo la kuchochea usimamizi endelevu wa Misitu Tanzania.

## Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Haki katika Misitu Tanzania


Awamu ya kwanza ya mradi ilitekelezwa kuanzia mwaka 2011 hadi 2015 katika kanda 6 za MJUMITA ambazo zinapatikana katika Wilaya 30, mikoa 13 ya Tanzania Bara, na zinahusisha Asasi za Kijamii (CBOs) 110 zenye wananchama 10,370 na vijiji 451 na kunufaisha takribani wananchi 1,029,215. Baadhi ya Mafanikio ya awamu ya kwanza ya mradi ni pamoja na:

- Wanajamii 904 (wanawake 452 na wanaume 452), takribani wajumbe 12,250 wa kamati za maliasili na halmashauri za vijiji kutoka katika asasi za kijamii (CBOs) 110 na vijiji 400 vinavyotekeleza mpango wa usimamizi Shirikishi wa Misitu Tanzania Bara walipata maarifa ya tathmini ya utawala bora katika usimamizi wa Misitu ya Vijiji. Serikali za Vijiji 300 ziliweza kufanya tathmini ya utawala bora ambao ulisaidia kuongeza ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji katika Halmashauri za Vijiji na Kamati za Maliasili;

- Misitu 6 yenye bioanuai muhimu kwa taifa ambayo ni Chome, Rondo, Pugu, Kazimzumbwi, Ruvu Kusini na Uduzungwa Scrap ilifanyiwa tathmini ya hali ya msitu; ambapo taarifa ya matokeo ya tathmini hiyo iliwasilishwa kwa wadau ambao walifanya maamuzi ya kuboresha usimamizi wa misitu hiyo.

- Mradi uliwezesha wanajamii kuchukua hatua za kisheria kuhusu jumla ya matukio 101 ya uharibifu wa misitu nchini. Matukio yaliyofikia hatua ya kupelekwa mahakamani na kuhukumiwa yaliongezeka kutoka asilimia sifuri mwaka mwa kwanza wa mradi, hadi asilimia 16.1 katika kipindi cha miezi 6 ya mwaka 2014;

- Mradi ulitoa mafunzo kwa wanajamii 300 kutoka katika kanda 6 za MJUMITA kuhusu viwango vya uthibitishaji misitu, na viwango vya MKUHUMI, na kusaidia kuongeza uelewa katika usimamizi endelevu wa misitu.




## Kwa nini Awamu ya Pili ya Mradi wa Haki katika Misitu?

Wazo la awamu ya pili la Mradi limetokana na uwepo wa changamoto mbalimbali katika sekta ya misitu, hususani misitu iliyo katika ardhi ya vijiji:

- Uwepo wa zaidi ya hekta milioni 17.6 za misitu katika ardhi ya vijiji, ambayo bado hazijatengwa kisheria kuwa Misitu ya Hifadhi ya Vijiji. Hii ni sawa na takribani asilimia 80 ya misitu yote iliyo katika ardhi za vijiji ambayo kwa ujumla ni takribani hekta milioni 22, yaani asilimia 46 ya ardhi ya misitu yote Tanzania;

- Zaidi ya hekta 469,000 za misitu hasa ile ambayo haijahifadhiwa katika ardhi za vijiji hupotea kila mwaka kutokana na kilimo holela na uvunaji haramu wa mazao ya misitu;

- Uwepo wa sera au matamko ya serikali yenye mwelekeo wa kuondoa maamuzi juu ya usimamizi wa Misitu ya Hifadhi za Vijiji kwenye mamlaka za serikali za mitaa, mfano GN 417, ya Mei 24, 2019, hali ambayo inaweza kupunguza motisha kwa wananchi kuhifadhi misitu iliyo kwenye ardhi ya vijiji.



## Lengo la mradi

Lengo kuu la Mradi wa Haki Katika Misitu ni kuongeza uwajibikaji kwa umma wa Tanzania (Jamii, serikali kuu na serikali za mitaa) katika kulinda rasilimali za kiikolojia, ambazo ni muhimu katika kupambana na mabadiliko ya tabia nchi na kuchochea maendeleo ya jamii.

**Kwa namna gani mradi utafikia malengo yake?**
Ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, mradi umejiwekea matarajio makuu matatu kama ifuatayo:

**Tarajio la kwanza:** Wananchi wengi zaidi kuelewa faida na kuwa na nguvu zaidi ya kulinda misitu iliyo katika ardhi za vijiji.

**Shughuli zitakazofanyika ili kufikia tarajio la kwanza:**

➢ Kuwajengea uwezo viongozi wa vijiji na jamii juu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii, utetezi na jinsia. Mafunzo yatatolewa kwa wanajamii na viongozi wa vijiji 1,000, ambao watawakilisha mitandao ya MJUMITA 30, vijiji takribani 100 katika kanda za Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini, na Kusini;

➢ Kuziwezesha asasi za kijamii (CBOs) na serikali za vijiji kuandaa mkakati na mpango wa uraghibishi/Utetezi kwa ajili ya kuhimiza uanzishwaji wa misitu mipya kwenye ardhi za vijiji, pamoja na kusimamia misingi ya utawala bora katika vijiji ambavyo vinatekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii;. Mradi utawezesha utekelezaji wa mpango huu, ikiwa ni Pamoja na kufanyika kwa vikao na wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya Kijiji, kata, wilaya na taifa kwa ajili ya kujadili na kutatua changamoto zilizopo;

➢ Kuwezesha vijiji vinavyotekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii kukabilina na matukio ya uvunaji haramu na uharibifu wa misitu kwa kuzingatia sheria. Mradi utaziwezesha serikali za vijiji kuchukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kisheria katika kufungua na kuendesha kesi zinazohusiana na uharibifu wa misitu ya vijiji.

**Tarajio la pili:** Kuhimiza Uwekezaji zaidi kwa ajili ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii Tanzania.

**Shughuli zitakazofanyika ili kufikia tarajio la pili:**

➢ Kufanya utafiti ili kuangalia fursa kwa serikali ya Tanzania kupata fedha kwa ajili ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Vijiji kupitia mifuko ya kimataifa ya kukabiliana na mabaliko ya tabia nchi;

➢ Kuwezesha Serikali kuandaa angalau maandiko mawili ya miradi yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 3, yenye lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kupitia Misitu ya Hifadhi za Vijiji;

➢ Kufanya ushawishi kupitia vyombo vya habari na kushiriki mikutano ya kimataifa ya kujadili mabadiliko ya tabia nchi (UNFCCC -CoP); ili fedha za mifuko ya kimataifa ziwekezwe zaidi katika kuendeleza Misitu ya Hifadhi za Vijiji kwa manufaa ya jamii za Tanzania.

**Tarajio la tatu:** Kufanya ufuatiliaji wa uharibifu katika misitu 3 yenye hadhi ya kitaifa na kimataifa na kuhakikisha uharibifu huo umepungua.

**Shughuli zitakazofanyika ili kufikia tarajio la tatu:**

- Kufanya utafiti kwa kushirikiana na wakala wa huduma za misitu Tanzania na wadau wengine juu ya vichocheo vya uharibifu misitu ya hifadhi asilia ya Mkingu, Chome na Uzungwa, pamoja na misitu ya vijiji;
- Kuandaa mikutano na wadau kujadili vichocheo vya uharibifu wa misitu na kuweka mikakati ya pamoja;
- Kuwezesha vijiji na wadau wengine kushiriki katika kuandaa mkakati wa kitaifa unaohusu Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii.

**Wadau wa utekelezaji wa mradi**

Wadau wakuu katika utekezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

- OR – TAMISEMI na Mamlaka za serikali za mitaa;
- Idara ya Misitu na Nyuki na Wakala wa huduma za misitu;
- Viongozi wa kuchaguliwa kama vile wabunge na madiwani
- Halmashauri za vijiji;
- Asasi za kijamii (CBO) na wanajamii kupitia hizo asasi hizo na serikali za vijiji.

**Sehemu mradi unatekelezwa**

Mradi wa Haki katika Misitu (FJT) unatekelezwa katika Kanda tatu za kitaifa za MJUMITA ambazo ni:

| Na | Kanda | Ofisi ilipo | Mikoa na Wilaya | Mawasiliano |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kanda ya Kaskazini | Korogwe Mjini | Mkoa wa Tanga katika wilaya za Mkinga, Muheza, Korogwe na Bumbuli; | 0768636735 Mratibu wa Kanda 0784812158 Mratibu Msaidizi wa Kanda |
| 2 | Kanda ya Nyanda za juu kusini | Iringa Mjini | Mkoa wa Iringa katika wilaya za Iringa, Kilolo na Mufindi; | 0754257247 Mratibu wa Kanda 073720 4424 Mratibu msaidizi wa kanda |
| 3 | Kanda ya Kusini | Kilwa Masoko | Mikoa ya Pwani (Rufiji), Lindi (Liwale, Mtama, Nachingwea na Kilwa) na Ruvuma (Tunduru). | 0752566586 Mratibu wa Kanda 0654898154 Mratibu msaidizi wa Kanda |

## Watekelezaji wa mradi

**Shirika la kuhifadhi misitu ya asili Tanzania (TFCG)**

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) ni shirika lisilo la kiserikali lenye maono ya kufidhi na kurejesha bioanuwai za misitu yenye umuhimu wa kimataifa Tanzania.

**Dhima ya TFCG:** Kupunguza umasikini kwa jamii za vijijini na kuhifadhi misitu yenye umuhimu kimataifa nchini Tanzania kwa manufaa ya vizazi vya sasa na baadaye.

**Kwa mawasiliano**
Website: www.tfcg.org
Email: tfcg@tfcg.or.tz

**Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA)**

MJUMITA ni Mtandao wa asasi za kijamii (CBO) zaidi ya 117 zinazoundwa na vijiji vinavyotekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu katika mikoa 13, Wilaya 30, zaidi ya vijiji 450 ikihusisha zaidi ya vikundi 500, na wananchama zaidi ya 10,000.

**Dhima ya MJUMITA:** MJUMITA inataka kuona jamii ya Tanzania inayojali, kutunza kiuendelevu na kunufaika na misitu ya asili.

**Kwa mawasiliano:**
Website: www.mjumita.org
Email: mjumitaorg@mjumita.org